Jumiko la Maliasili Tanzania

Tanzania Natural Resource Forum

*HABARI JUU YA WANYAMAPORI KATIKA TANZANIA*

**Wanyamapori kwa watanzania wote: Kusimamisha upotevu, kuendeleza raslimali na kupanua mafao**

# MAPENDEKEZO YA KISERA ILI KUENDELEZA WANYAMAPORI WA TANZANIA

Umakini wa kimataifa umeelekezwa kwa wanyama wa Tanzania kwa sababu ya uhifadhi wa bioanuai, lakini hapa kwetu Tanzania suala katika usimamizi wanyamapori ni muhimu kwa sababu ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Wanyamapori Tanzania ni raslimali muhimu mno kwa ukuaji wa uchumi na utalii wa kupiga picha, na pia kwa kiwango kidogo kwa uwindaji wa kiutalii

***Wanyamapori huipatia Tanzania soko lenye ushindani katika ulimwengu wa leo wenye utanda wazi ambapo hakuna raslimali nyingine inayoweza kutoa.***

Wanyamapori ni raslimali endelevu ikiwa Tanzania itaandaa sera na matendo yenye usimamizi endelevu wa wanyamapori, shughuli za kiuchumi zinazotokana na wanyamapori zitaendelea kukua na kupanuka kwa miongo mingi ijayo.

Cha kusikitisha ni kwamba wanyamapori wa Tanzania wanapotea, na hivyo kupoteza ushindani katika soko la kikanda kama vile Namibia au Botwana ambako wana idadi ya wanyama inayoongezeka ama iliyotulia, na ambako pia kuna utalii wenye nguvu unaokua hasa ule wa uwindaji na wa upigaji picha.

Ili watunga sera watanzania waweze kujibu changamoto za uendelezaji sera endelevu za usimamizi wa wanyamapori, vigezo kadhaa lazima vitambuliwe.

1. Tanzania imeanzisha mtandao mkubwa wa maeneo yaliyohifadhiwa - Hifadhi za Taifa, Mapori ya Akiba na Misitu ya Hifadhi - na imeongeza kiwango cha ardhi ambacho kiko chini ya namna hii au ile ya hifadhi.

2. Wanyamapori wanaendelea kupungua kwa sababu hata hifadhi na mapori makubwa yameungana na ardhi nje ya mipaka yao, na wanyama huondokea kupita mipaka na kwenda mahali ambako hawapati ulinzi kwa sababu ya upungufu wa raslimali za serikali na kukosekana motisha za uhifadhi kwa jamii.

3. Changamoto ni muhimu kuandaa sera zinazohimiza uhifadhi maeneo ya jamii na yale ya binafsi nje ya maeneo makuu yaliyohifadhiwa. Cha muhimu zaidi na kinachohusiana na muundo wa sera na maendeleo ni kwamba sera lazima ziwe na mtazamo wa kuhusisha wanyamapori na wamiliki wa ardhi nje ya hifadhi hizo.

Mwalimu J.K. Nyerere katika tamko la Arusha mwaka

*Kwa kushirikiana na*

policy forum

WILDLIFE CONSERVATION SOCIETY

WWF

PINGO's FORUM

WILDLIFE CONSERVATION SOCIETY OF TANZANIA

*© JMT 2008*

1961 alisema:

***"Uhai wa wanyamapori ni jambo linalotuhusu sana sote katika Afrika. Viumbe hawa wa porini, wakiwa katika mapori wanamoishi, sio muhimu tu kwa ajili ya kuajabiwa na kuvutia lakini pia ni sehemu ya maliasili yetu na pia ndio mustakabali wa maisha yetu ya baadaye. Kwa kukubali dhamana ya wanyamapori wetu tunatamka kwa dhati kwamba tutafanya kila tuwezalo kuhakikisha kwamba wajukuu wa watoto wetu wataweza kufurahia urithi huu mkubwa na wa thamani adimu."***

Kipindi cha miaka ya 1990 Wizara ya Maliasili na Utalii Tanzania ilifanya tathmini ambayo ilihitimisha kwamba:

***"Ni muhimu kwa uhifadhi wa wanyamapori hapo baadaye kwa hapa Tanzania wananchi waishio pamoja na wanyamapori wapatiwe mafao ya moja kwa moja yatokanayo na wanyama."***

Na hii ndiyo ilikuwa fikirio kubwa katika Sera ya Wanyamapori Tanzania ya mwaka 1998 na msukumo katika kuweka wanyamapori wawe na ushindani kama moja ya matumizi ya ardhi ambako maeneo ya WMA yangeanzishwa na wananchi kuwa na mamlaka kamili juu ya wanyamapori katika maeneo hayo.

Sera hii ilijengwa katika ukweli wa kiuchumi kwamba ili wanyama wahifadhiwe nje ya maeneo ya hifadhi ni lazima walete manufaa ngazi ya vijiji, kama uzoefu unavyoonesha Tanzania na katika nchi nyingine mashariki na kusini mwa Afrika.

Kipindi cha miaka kumi iliyopita, misingi ya sera ya wanyamapori ya mwaka 1998 haijatekelezwa:

- ⇨ Maeneo ya WMA yamebuniwa kwa njia ambayo inakuwa ni vigumu kuyaanzisha na ambayo haitoi haki za uwazi kwa jamii kunufaika kutokana na wanyamapori.
- ⇨ Mikataba yenye manufaa kati ya vijiji na wawekezaji, kwa bahati mbaya imekuja kuwa na mgongano na uwindaji wa kiutalii nayo imedumu lakini ingeweza kuwa imetatuliwa.
- ⇨ Migongani ya umiliki wa ardhi kutokana na mwingiliano wa tafsiri wa maeneo ya vijiji na Mapori Tengefu (GCA) imesababisha uhasama na kudhoofisha umiliki na usalama wa ardhi ngazi ya jamii.
- ⇨ Uwindaji wa kitalii haujasimamia kwa njia ambayo ni shindani wala hauko wazi ambayo ingekuza pato la kitaifa, na kwa mwaka uliopita migogoro ilijitokeza juu ya upangaji bei ya maeneo ya uwindaji.

Masuala haya yote ni kitovu cha kuendeleza wanyamapori Tanzania na mchango katika maendeleo ya kiuchi ya Taifa na kupunguza umaskini.

Ili kuchangia katika jitihada za watunga sera, wadau wote wa kiserikali na wale wasiowa kiserikali na ili wanyamapori wawe na faida kwa kizazi cha sasa na kizazi kijacho, mapendekezo yafuatayo ya kisera yamewekwa kufuatia habari za kiutafiti katika machapisho sita yaliyotangulia.



*Twiga katika tafakuri - ni nembo ya Taifa Tanzania*

## 1. KUREKEBISHA SHERIA NA SERA YA WANYAMAPORI ILI KUKABILI CHANGAMOTO ZA SASA NA KUUNDA MFUMO WA KITAASISI KWA AJILI YA USIMAMIZI ENDELEVU WA WANYAMAPORI TANZANIA

Changamoto nyingi Tanzania kuhusiana na idadi ya wanyamapori na kuhakikisha mafao ya wanyamapori yanaongezeka siku za usoni zinaweza tu kujibiwa kupitia mabadiliko ya kisheria. Tanzania, kwa miaka mingi, imekuwa ikiandaa sheria ya wanyamapori na sheria hii inatarajiwa kwenda Bungeni sasa.

Ni watu wengi wangependa kufanya kazi pamoja na serikali ili kuona wanyamapori wa Tanzania wanafikia uwezo wa juu wa kuwa ni raslimali endelevu ya kiuchumi katika nchi. Na ni dhahiri kuwa njozi hii kwa sasa iko katika matishio. Wanasiasi ni budi wapate ushauri, wasikilize na kutumia taaluma, uzoefu na usaidizi wa mashirika huru na yale ya binafsi ili kufikia matokeo tarajiwa. Na kiini katika hili kuna hitaji la kujenga ubia imara, kwa misingi ya kushirikiana na kuaminiana, kupitia, kutambua na kuheshimu nafasi tofauti na majukumu ya serikali, mashirika huru na sekta binafsi.

***Sheria hii mpya ya wanyamapori iliyoandaliwa Tanzania inahitaji na ni muhimu kufanya yafuatayo ili iweze kujibu kwa ufanisi changamoto za sasa zinazoikabili sekta ya wanyamapori nchini:***

***Kwanza, itapaswa kuhimiza upatikanaji wa mafao kuwafikia wananchi kutokana na wanyamapori. Na mafao hayo yanatakiwa yatolewe kisheria na si kufuata kanuni zinazotolewa na Wizara.***

***Pili, ni budi itoe matumizi zaidi ya wanyamapori kupitia mfumo wa usimamizi wa uwindaji wa kitalii ambao uko wazi, ni shindani na ambao una kiwango sahihi cha ufuatiliaji.***

***Tatu, lazima ihimize ushirikishwaji jamii, ushauri, na haki ya kupata habari kutoka sekta ya wanyamapori, ikiwa ni pamoja na uandaaji wa sera na sheria za serikali.***

---

## 2. KUBORESHA NA KUFAFANUA KANUNI ZA UANZISHWAJI MAENEO YA HIFADHI ZA JAMII (WMA) KATIKA ARDHI ZA VIJIJI

**Jambo moja na la muhimu** katika kuendeleza wanyamapori wa Tanzania ni kuanzisha motisha zenye tija kwa ajili ya jamii ili kusaidia uhifadhi. Motisha hizo zinaweza tu kuanzishwa kwa kuwawezesha wananchi kuelewa thamani ya kiuchumi ya wanyamapori. Maeneo ya WMA ndiyo mfumo muhimu wa kulifikia hili, lakini muundo wa WMA ni budi uboreshwe ili kufanya uanzishwaji wa WMA uwe rahisi na kwamba jamii ni wafaidikaji wakuu wa mazao na huduma za WMA, kwa vile wanajamii tayari wanaishi na wamebeba gharama za wanyamapori katika maeneo yao ya vijiji.

***Vipaumbele katika kuboresha kanuni za WMA ni:***

- ⇨ ***Kupunguza masharti ya uanzishaji WMA kwa jamii;***
- ⇨ ***Kanuni zifafanue utaratibu wa ugawanaji mafao katika WMA, ili kuhakikisha kwa asilimia 75 ya mapato kutoka WMA inabaki ngazi ya vijiji;***
- ⇨ ***Kuhakikisha kuwa vijiji wanapewa maamuzi ya kisheria kulingana na uwekezaji katika WMA, ikiwa ni pamoja na kuamua ni makampuni yapi ya uwindaji wa kitalii yaruhusiwe kuwinda katika maeneo hayo;***
- ⇨ ***Maeneo ya WMA yawianishwe na maeneo ya ardhi ya misitu ya vijiji ili jamii wapate manufaa ya juu kutokana na maliasili katika ardhi za vijiji. Mtazamo wa kisera unahitajika.***

Mapendekezo haya yamefanywa ili kuwezesha uanzishwaji wa WMA ambazo zitawapa jamii faida kubwa na ya uhahika kupitia wanyamapori, na hivyo kusababisha jamii kupenda uhifadhi na kukuza mchango wa wanyamapori katika kupunguza umaskini.

## 3. KUSAIDIA NJIA MBADALA ZA KUWANUFAISHA WANANCHI KUTOKANA NA WANYAMAPORI KUPITIA UTALII WA BIASHARA-UBIA ZA JAMII NA SEKTA BINAFSI

Wakati wa uanzishwaji wa WMA umekuwa ni changamoto kwa miaka 10 iliyopita, mifano ya sasa ya kufaidisha wananchi kutokana na wanyamapori pia inapatikana katika mikataba ya vijiji na wawekezaji wa sekta binafsi. Tangu mwanzoni mwa miaka ya 1990, vijiji vingi vimejihusisha na utalii kwa kutoa maeneo kwa makampuni binafsi katika ardhi zao ili waweze kupata kodi ya uwekezaji. Makubaliano hayo yanasimamiwa na mikataba ya kisheria ikihakikisha vijiji na halmashauri za wilaya wanapata maduhuli kutokana na utalii wa wanyamapori. Makubaliano hayo yamefanyika kisheria chini ya Sheria ya Serikali za Mitaa (1982) na Sheria ya Ardhi ya Vijiji (1999).

Loliondo ni mfano wa pekee ambako vijiji saba sasa wanapata zaidi ya dola za kimarekani 300,000 (TZS milioni 360 kwa mwaka). Mafao hayo yamefikiwa bila kupitia mchakato changamano wa kuanzisha WMA. Hakuna haja ya kuanzisha WMA katika maeneo hayo ambako jamii wanapata faida kutokana na utalii wa wanyamapori, mipango ya matumizi ya ardhi ipo na raslimali ya wanyamapori iko salama. Malengo yote ya kiuhifadhi na yale ya uchumi wa jamii yanafikiwa katika mfumo huu.

Kuruhusu jamii ifaidike kwa njia mbalala kutokana na wanyamapori itaruhusu ubunifu katika mipango ya kiuhifadhi. Mfano wa hivi karibuni, ni wa ardhi iliyotengwa kwa hiari ya jamii kwa ushirikiano wa wamiliki wa hoteli, makampuni ya utalii na vijiji huko Simanjiro - ikiwa ni sehemu wa mfumo ikolojia wa Tarangire. Vijiji vimekubali kulipwa ili kuacha maeneo haya kwa ajili ya mifugo na kuzuia kilimo kwa lengo pia la kulinda maeneo ya kuzalia nyumbu.

Katika maeneo mengi utalii huu wa jamii na sekta binafsi unaendelea kuwa ni chombo cha muhimu kwa utalii wa Tanzania, na pia kuchangia katika malengo ya Taifa ya kukuza biashara ya utalii. Hata hivyo, biashara hizi hazijapata baraka za watunga sera wa sekta ya wanyamapori katika miaka 10 iliyopita, hata maeneo kama Tarafa ya Loliondo ambako mwanzoni biashara yao ilikubalika na wote (Idara ya Wanyamapori na TANAPA). Biashara hizi zinaendana na sera zingine za serikali kama vile MKUKUTA ambayo inahimiza pato kwa jamii kutokana na utalii wa wanyamapori.

Kukosekana kwa ukubali kunatokana na sababu mbili:

1. Biashara za kitalii sehemu nyingine zimeleta migogoro na maeneo ya uwindaji wa kitalii yaliyotolewa na Idara ya Wanyamapori katika maeneo hayo.
2. Katika mwaka 2007 Wizara ya Maliasili na Utalii ilitoa kanuni za utumiaji wanyamapori usio wa uvunaji ambazo ziliweka mfumo wa ada unaohitaji ada nyingi zilipwe Idara ya Wanyamapori.

Kama kanuni hizi zitatekelezwa bila kuwa na mfumo wa kugawana mapato ambao ni ya moja kwa moja wenye kujitosheleza, wenye kuona mbali vijiji ambavyo vilikuwa vinapata faida ya moja kwa moja vitapoteza mapato viliyoyapata kwa miaka mingi. Hii haitakuwa na mkito mzuri ama kwa kupunguza umaskini, kukuza utajiri au motisha kwa jamii ili kuhifadhi wanyamapori. Kwa hiyo, itaongeza juu ya matatizo yanayoikabili sekta ya wanyamapori kwa sasa.

Inasemekana kwamba uhalalishwaji wa kanuni za matumizi ya wanyamapori una misingi ya katika fikra za kuwa makampuni ya utalii yanalipa fedha kidogo kwenye vijiji. Hata hivyo, kwa kurudisha ukusanyaji wa ada serikali kuu haitazuia malipo hayo pungufu kwa vijiji. Badala yake kwa kusaidia soko shindani itaviwezesha vijiji kupata mafao ya kiwango cha juu katika sekta binafsi. Nafasi ya serikali ni kutoa uangalizi ili kuhakikisha soko linaendelea vizuri na kuhimiza mipango ya biashara bunifu.

Migongano ya kisera na matendo ni dhahiri haiko katika dhamira ya kitaifa, wala watu wake na raslimali ya wanyamapori, na hitilafu hii ni lazima ikabiliwe.

## 4. KUKUZA THAMANI YA UCHUMI WA WANYAMAPORI KWA KUANZISHA MFUMO WA USHINDANI KATIKA UGAWAJI WA VITALU VYA UWINDAJI KAMA VILE ILIVYO KATIKA ZABUNI AU MINADA YA WAZI.

Uwindaji wa kiutalii ni wa muhimu kama matumizi ya wanyamapori, na ni muhimu kwa mfumo wa usimamizi wa uwindaji kitaifa, ni endelevu na huhakikisha inakuza manufaa ya kiuchumi ya raslimali ya wanyamapori. Mfumo wa sasa wa ugawaji maeneo ya uwindaji na upangaji wa bei kiutawala haufanyi hilo.

***Ni mfumo tu wa uwazi wenye ushindani katika kugawa vitalu vya uwindaji utahakikisha nchi inapata bei ya juu iwezekanavyo kwa maeneo ya uwindaji.***

Na hii ndiyo sababu nchi zingine zote katika Afrika zinatumia mfumo wa uwazi na masoko shindani ili kugawa maeneo ya uwindaji, na ndiyo maana mfumo huu unatambulika kimataifa kuwa ndiyo bora kwa kusimamia uwindaji wa kitalii.

Kanuni ya uwazi na zabuni zenye ushindani ndiyo msingi wa utaratibu na mfumo wa kitaifa Tanzania wa kufanya manunuzi ya huduma au vifaa kama ulivyofafanuliwa katika Sheria ya Manunuzi ya Serikali.

Hata hivyo, wakati zabuni zilizowazi na zenye ushindani kuhusu uwindaji ndiyo njia nzuri, umakini unatakiwa uwekwe ni kwa jinsi gani jamii watachagua nani awinde katika ardhi yao. Moja ya uwezekano ni kuwa na shirikisho la maeneo ya WMA la asasi zilizoidhinishwa (AA) zikinadi katika maeneo ya WMA, wakati Idara ya Wanyamapori itanadi vitalu vya uwindaji katika Mapori ya Akiba—kukiwa na misingi na miongozo inayolingana. Uzuri wa mfumo huu ni kwamba utasaidia kutatua migogoro baina ya vijiji na baadhi ya makampuni ya uwindaji. Lakini chaguzi zingine zaweza kufaa pia.

***Katika kukuza pato la uchumi kitaifa kutokana na wanyamapori, ni vizuri kufikiria ni biashara gani ya wanyamapori ifanyike katika maeneo tofauti, kwa kutumia takwimu za pato la kiuchumi la wanyamapori katika eneo moja (angalia Chapisho Na. 3). Kufuatia ukuaji wa utalii kaskazini mwa Tanzania kwa kipindi cha miaka 20 iliyopita, uzalishaji kwa hekta moja kutokana na utalii wa picha umekuwa mkubwa kuliko uwindaji wa kitalii katika maeneo mengi. Hivyo haileti maani kiuchumi kuendesha biashara ya uwindaji pekee katika maeneo fulani mathalani ardhi kuzunguka Hifadhi za Tarangire na Serengeti ambazo zina thamani kubwa katika utalii wa picha. Mwenendo unaofanana umejionyesha katika kanda ya utalii kusini mwa Tanzania, na watunga sera, wanahitaji kuwa macho katika ujanja wa kutenga maeneo ya uwindaji kinyume na kutenga maeneo ya utalii wa picha.***

## 5. SERIKALI IONGEZE MAPATO YA HAZINA KUU KUTOKANA NA WANYAMAPORI IKITILIA MKAZO UKUSANYAJI WA MAPATO YA UTALII – HASA KODI ZILIZOPO, NA KUHAKIKISHA JAMII NA WAMILIKI WA ARDHI BINAFSI WAKIPATA MAPATO YA MOJA KWA MOJA KAMA VILE ADA ZA MAENEO YA UWINDAJI NA UTALII WA PICHA

Jambo muhimu kwa ajili ya wanyamapori Tanzania ni kuhakikisha ugawanaji sawia wa mapato ili wanyama waongezeke, wahifadhiwe na wadau wote, na thamani ya kitaifa ya biashara ya wanyamapori itaongezeka.

***Serikali kuu iwe ndiyo mwangalizi wa wanyamapori nje ya maeneo makuu yaliyohifadhiwa, na sio msimamizi mkuu wa wanyamapori nje ya maeneo yaliyohifadhiwa na mwelekezaji wa mapato yake kama ilivyo sasa. Hii itasaidia kukuza mapato katika kipindi cha kati kwa wote serikali na jamii kuliko kuendelea mfumo uliopo sasa.***

Serikali itakuwa na uwezo wa kuongeza pato lake kwa kuzingatia sera zenye tija katika kutoza kodi na kuhimiza uwekezaji wa biashara ya utalii, wakati wananchi wakiwezeshwa kupata maduhuli kutokana na utalii na maeneo ya uwindaji na hivyo kuendeleza na kukuza hazina ya raslimali ya wanyamapori nje ya maeneo yaliyohifadhiwa.

---

## 6. KUTATUA MIGOGORO BAINA YA USIMAMIZI WA WANYAMAPORI NA HAKI ZA ARDHI YA JAMII

Sehemu kubwa za nchi zimetengwa zikiingiliana ardhi zilizohifadhiwa na ardhi za vijiji kama matokeo ya kuwepo kwa Mapori Tengefu (GCA). Mapori haya Tengefu hayajawahi kuwa kundi la usimamizi wa wanyamapori wenye tija, na hakuna makatazo juu ya shughuli za kibinadamu au makazi isipokuwa uvunaji wa wanyamapori. Na kwa sababu hiyo, **Mapori Tengefu hayaongezi thamani kwa namna yoyote ile kwa uhifadhi wa wanyamapori**. Hii ni kwa sababu maana pekee ya Mapori Tengefu ni kwamba wanyamapori hawawezi kuvunwa bila leseni ya serikali; lakini wanyamapori popote pale Tanzania hawawezi kuvunwa bila leseni.

Kwa hiyo, **Mapori Tengefu hayakidhi kusudi lolote lenye maana ya minajiri ya uhifadhi**. Hili ni hitimisho la tathmini ya Wizara, sekta ya wanyamapori mwaka 1995 kuhusiana na Mapori Tengefu, na hii ndiyo maana Sera ya Wanyamapori ya mwaka 1998 ilipendekeza Mapori yote Tengefu yapandishwe ngazi kuwa Mapori ya Akiba au yabadilishwe kuwa maeneo ya WMA.

Hata hivyo, sawa na mapendekezo mengine yaliyotolewa muongo mmoja uliopita, maoni haya hayajatekelezwa, na hadi leo mwingiliano wa Mapori Tengefu na ardhi za vijiji huleta migogoro na kudhofisha uhakika wa kumiliki ardhi kwa wananchi walio wengi.

***Mapori Tengefu (GCA) hayakidhi kusudi lolote la uhifadhi wa wanyamapori, na huleta migogoro kwa haki za ardhi kwa wanajamii. Mapori yote Tengefu ingefaa yafutwe. Ufutwaji wa Mapori Tengefu hautakuwa na madhara yeyote kwa uhifadhi wa wanyamapori, na kutakuwa na mkito chanya kwa umiliki wa ardhi kijamii na kurahisisha uanzishwaji wa maeneo ya WMA kama ubunifu wa kiuhifadhi na kiuchumi.***